www.freekcsepastpapers.com www.freekcsepastpapers.com www.freekcsepastpapers.com

# MTIHANI WA MWIGO WA LANJET 2022

**MUHULA WA PILI 2022**

**102/2**

**KISWAHILI**

**KARATASI YA PILI**

**MUDA: SAA 2 ½**

**JINA ……………………………………………………………………… NAMBARI ……………… DARASA ___________**

**MAAGIZO:**

- **Karatasi Hii Ina Sehemu Nne.**
- **Ni Sharti Mtahiniwa Ashughulikie Sehemu Zote.**
- **Maswali Yote Yajibiwa Kwa Lugha Ya Kiswahili.**

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |

free exams at www.freekcsepastpapers.com

**1. UFAHAMU**

**Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuatia.**

Vipindi mbalimbali vya historia vimeshuhudia kuibuka kwa magonjwa ya ajabu. Magonjwa hayo yamehangaisha watu na kuzishughulisha bongo za wanasayansi na madaktari katika kutafuta tiba. Magonjwa kama vile tauni, kifua kikuu, homa ya matumbo na ndui ni baadhi ya yale yaliyotisha sana nyakati fulani za historia ya binadamu. Magonjwa haya yaliwaua maelfu ya watu na kutibua mifumo na taratibu za maisha ya watu.

Hata hivyo magonjwa hayo yaliweza kuchunguzwa na kutafutiwa tiba kabla ya kumaliza kabisa kizazi cha binadamu. Lakini hii ni baada ya kuwasukuma maelfu ya watu kaburini. Ulimwengu wa sasa unashuhudia janga jingine la maradhi sugu ya Ukimwi. Neno "UKIMWI" lilitoholewa kutokana na athari za ugonjwa huo mwilini. Neno "UKIMWI" humaanisha <u>Ukosefu wa Kinga Mwilini</u>, ambapo herufi za kwanza za maneno matatu ziliunganishwa pamoja na kuunda neno hilo. Ugonjwa huu ambao tayari umewaua mamilioni ya watu kote ulimwenguni unazidi kuenea kwa kasi, mfano wa moto katika kichaka. Kutokana na kasi yake ya kuua watu, ugonjwa wa UKIMWI umepewa majina kama vile



www.freekcsepastpapers.com www.freekcsepastpapers.com www.freekcsepastpapers.com

www.freekcsepastpapers.com www.freekcsepastpapers.com www.freekcsepastpapers.com
'umeme' na pia 'ugonjwa wa vijana'. Watu wengi wanaoambukizwa virusi vya UKIMWI ni wale walio na miaka kati ya 15 hadi 49. Kundi hili kwa kweli ndilo, linalohesabiwa kuwa na nguvu za kutunza jamii kwa njia nyingi. Iwapo wengi katika kundi hili watakumbwa na maradhi haya, watasalia wakongwe na watoto wasioweza kujimudu.

Nchini Kenya, UKIMWI uligunduliwa kwa mara ya kwanza mnamo mwaka wa 1984. Kufika mwezi wa Juni 1996, inakisiwa kuwa ugonjwa huu ulikuwa umewaua watu wapatao 65,647 nchini . Hivi sasa, inasemekana kuwa takriban watu zaidi ya 500 hufa kila siku nchini Kenya kutokana na janga hili. Aidha, imethibitishwa kwamba takriban wafu milioni mbili u nusu tayari watapoteza maisha yao kutokana na kuambukizwa virusi vya ugonjwa huu humu nchini. Maradhi haya sasa yamekuwa janga la kitaifa.

Kutokana na kuongezeka kwa visa vya UKIMWI, hospitali na zahanati nyingi kote nchini zinashindwa kukidhi mahitaji ya wagonjwa. Kwa hivyo makundi ya kujitolea na mashirika mbalimbali yameundwa ili kuwahudumia wagonjwa wa UKIMWI. Baadhi ya makundi hayo hutoa tiba ya kisaikolojia pamoja na kuwapa ushauri wa hima ya kuishi, badala ya kukata tamaa. Wagonjwa wengi pia huishia kutibiwa nyumbani kwao.

Lakini jambo la kuzingatia ni hili, tujifunze kutokana na historia. Tuwe na matumaini kwamba siku moja tiba ya ugonjwa huu itapatikana. Hii ni kwa sababu tumethibitishiwa haya kutoka katika historia yetu wenyewe. Ikiwa magonjwa yaliyosababisha vifo vya wengi kutokana na ukosefu wa tiba yalitokomezwa kupitia juhudi za kimatibabu, sembuse huu ugonjwa tulio nao sasa? Huku tukijikinga kutokana na maradhi haya tusife moyo bali tuwe na matumaini kwani subira huvuta heri.

free exams at www.freekcsepastpapers.com

**Maswali**

a)Fafanua maana ya vifungu vifuatavyo

i) Kutibua mifumo na taratibu za maisha ya watu. (Alama 1)

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

ii) Kuwasukuma maelfu ya watu kaburini. (Alama 1)

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

b) Eleza aina ya magonjwa yafuatayo:-

i) Homa ya matumbo (Alama 1)

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

ii) Kifua Kikuu (Alama 1)



www.freekcsepastpapers.com www.freekcsepastpapers.com www.freekcsepastpapers.com

www.freekcsepastpapers.com www.freekcsepastpapers.com www.freekcsepastpapers.com

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

c) Kwa nini ugonjwa wa UKIMWI umepewa majina ya kimajazi? (Alama1)

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

d) Eleza madhara yoyote matatu ya UKIMWI kulingana na taarifa (Alama3)

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

e) Ni harakati zipi zinazoendelezwa kukumbana na janga hili? (Alama2)

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

f) Eleza mienendo inayopaswa kuendelezwa kuondoa kukata tamaa (Alama3)

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika taarifa.

i) Takriban ……………………………………………………………………………… (Alama 1)

ii) Hima ya kuishi ……………………………………………………………………… (Alama 1)

free exams at www.freekcsepastpapers.com

**2. MUHTASARI** (Alama 15)

Tunapinga na kulaani vikali visa vya ugaidi vinavyoendelea kutetemesha usalama wa wananchi.Hivi ni vitendo vya kinyama vinavovyotekelezwa na watu waliokosa ubinadamu na utu kabisa.Inakera mno kwa vitendo vya kigaidi .Inagadhabisha kuona Wakenya wasio na makosa wakiteswa na kuuwawa kinyama bila huruma na watu wasio na utu. Hatuogopi wala hatuna fedheha kuamba magaidi hawa wameelaaniwa na siku zao zimehesabiwa hapa duniani, damu ya mwananchi asiye na makosa katu watailipia. Napinga vikali pale magaidi hawa wanapohusisha vitendo hivi kuwa vita vya kidini, vita hivi si vya kidini kwani hakuna dini yoyote iliyo na imani ya kumwua kinyama binadamu asiye na makosa.

Kando na tishio la ugaidi, Wakenya pia wanakabiliwa na hatari za ujambazi, mauji, unajisi, ubakaji na maovu mengine. Katika juhudi za kudumisha usalama, polisi wana jukumu la kutumia kila mbinu kuhakikisha kuwa haki ya kikatiba ya Wakenya kuhusu kulindwa kwa maisha na mali yao. Lakini cha kusikitisha ni kuwa, mbinu ambazo polisi wamekuwa wakitumia hasa ile ya kufanya misako



www.freekcsepastpapers.com www.freekcsepastpapers.com www.freekcsepastpapers.com

www.freekcsepastpapers.com www.freekcsepastpapers.com www.freekcsepastpapers.com

inayoishia kuwanasa mamia ya raia wasio na habari kinachoendelea, inawaongezea Wakenya mateso. Hali hii inawaacha kwenye hatari ya kunaswa na majambazi ama polisi.

Matumizi ya mbinu hii ya misako imeishia kunasa raia wengi wasio na makosa.Wanaponaswa, hurundikwa kwenye seli usiku mzima ama siku kadha na hata kama wanaaachiliwa huwa tayari wameteseka. Huu ni ukiukaji wa haki za raia. Kadhalika, mbinu hii yanaonekana kama hila ya polisi kutaka kuonyesha wanafanya kazi lakini sio mwafaka kwani wanapokuwa wakiwanasa raia mijini na mitaani, magaidi na majambazi wanaendelea na shughuli zao.

Badala ya kusaka wakora kwa kubahatisha kwenye umati, polisi wanapaswa kubuni njia ambazo zitawapa mwelekeo mwafaka zaidi kuhusu wahalifu ili waweze kuwafuatilia. Ushirikiano baina yao na majasusi uwepo. Hii itawezesha polisi kupata habari muhimu kuhusu vitisho vya uhalifu. Maafisa wa usalama pia wanaweza kupata habari muhimu kutoka kwa raia.

**MASWALI**

(a) Ni nini maoni wa mwandishi kuhusu suala la ugaidi. (alama 7, 1 utiririko)

(maneno 60-70)

**Matayarisho**:

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................

**Nakala safi**

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................

(b) Kwa kutumia maneno yasiyozidi 50 fupisha aya mbili za mwisho. (alama 6, 1 utiririko)

**Matayarisho:**

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

free exams at www.freekcsepastpapers.com



www.freekcsepastpapers.com www.freekcsepastpapers.com www.freekcsepastpapers.com

www.freekcsepastpapers.com www.freekcsepastpapers.com www.freekcsepastpapers.com

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

**Nakala safi**

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

**3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)**

(a) Kipashio kikubwa zaidi katika ujenzi wa lugha kinaitwaje? (alama 1)

………………………………………………………………………………………………

free exams at www.freekcsepastpapers.com

(b) Andika sauti mbili ambazo ni vikwamizo vya mdomo na meno. (alama 2)

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

(c) Badilisha sentensi ifuatayo iwe katika usemi wa taarifa. (alama 2)

"Nitawafundisha usemi wa taarifa kesho," mwalimu alituambia.

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

(d) Tunga sentensi moja ukitumia kielezi cha nomino. (alama 2)

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………



www.freekcsepastpapers.com www.freekcsepastpapers.com www.freekcsepastpapers.com

www.freekcsepastpapers.com www.freekcsepastpapers.com www.freekcsepastpapers.com

(e) Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya matawi. (alama 4)

Wanafunzi wenye bidii masomoni hufuzu mtihani.

(f) Bainisha shamirisho katika sentensi ifuatayo: (alama 3)

Baba alipashwa habari kwa rununu.

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

(g) Tambua muundo wa virai vilivyopigiwa mstari katika sentensi zifuatazo: (alama 2)

Mikakati iliyobuniwa na serikali itaimarisha usalama nchini.

…………………………………………………………………………………………………………………

(ii) Mara nyingine msimu wa masika umewadia.

…………………………………………………………………………………………………………………

(h) Andika upya sentensi zifuatazo kwa kuzingatia kauli zilizomo mabanoni. (alama 2)

Watoto wenyewe wamekunywa maziwa yao yote. (tendwa)

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

(i) Pombe haramu inawafisha Wakenya wengi. (Badilisha kitenzi kiwe nomino)

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

(j) Tunga sentensi mbili tofauti kuonyesha matumizi yafuatayo ya **ndivyo**. (alama 2)

(i) Jinsi

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

free exams at www.freekcsepastpapers.com



www.freekcsepastpapers.com www.freekcsepastpapers.com www.freekcsepastpapers.com

www.freekcsepastpapers.com www.freekcsepastpapers.com www.freekcsepastpapers.com

(ii) Kirejeshi cha kuthibitisha.

………………………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………………………

(k) Eleza maana tatu zinazoibuliwa na vitate vilivyotumika katika sentensi hii. (alama 3)

Bosi wetu ana pozi nyingi lakini ni bozi sana.

………………………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………………………

(l) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya ukubwa.

Uso wa kijana yule ulichujuka alipoanguka. (alama 2)

………………………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………………………

(m) Eleza matumizi **mawili** ya viakifishi vifuatavyo: (alama 4)

Herufi nzito (H) / zilizokolezwa.

………………………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………………………

Mstari

………………………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………………………

free exams at www.freekcsepastpapers.com

(n) Bainisha mofimu za: (alama 3)

Nitakujia

………………………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………………………

(o) Unganisha sentensi hizi kwa kutumia kirejeshi cha kati mwafaka. (alama 1)

Gari limeibwa.

Gari ni langu.

(p) Ainisha vihusishi katika sentensi hizi: (alama 2)

(i) Mwanafunzi huyu ni mwerevu sana kuliko wenzake wote.

………………………………………………………………………………………………………………………………

(ii) Tangu apate mamlaka amepuuza wadogo wake.

………………………………………………………………………………………………………………………………



www.freekcsepastpapers.com www.freekcsepastpapers.com www.freekcsepastpapers.com

www.freekcsepastpapers.com www.freekcsepastpapers.com www.freekcsepastpapers.com

(q) Unda kitenzi kutokana na neno"Zawadi" (alama 1)

…………………………………………………………………………………………………………………………

(r) Bainisha vishazi katika sentensi ifuatayo: (alama 2)

Ingawa amefunga bao hajacheza kwa muda.

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

(s) Kanusha katika hali ya wingi. (alama 2)

Uovu alionionyesha ulinikera.

…………………………………………………………………………………………………………………………

**4. ISIMU JAMII (Alama 10)**

**" Maafisa 3 wakana kusaidia mshukiwa wa mauwaji ya watoto kutoroka kituoni.**

Maafisa watatu wa polisi jana walikana mashtaka ya kumsaidia mshukiwa wa mauaji ya watoto 13 kutoroka kutoka kituo cha polisi…**"**

(a) Huku ukitoa sababu mbili, tambua sajili hii. ( alama 3)

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

(b) Fafanua sifa zozote saba za sajili hii. (alama 7)

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

**© Mtihani wa Mwigo wa LANJET 2022**

**IDARA YA LUGHA**

**Kila La Heri !**

free exams at www.freekcsepastpapers.com



www.freekcsepastpapers.com www.freekcsepastpapers.com www.freekcsepastpapers.com